Wakulima Wadogo Wadogo wa Chai Nchini Sri Lanka Wabadilika kuwa Wasimamizi wa Ardhi Wanaotumia Mbinu Endelevu za Ukulima

Imeandikwa na Stella Paul

Mkulima mdogo wa chai Kamakandalagi Leelavathi anachuna majani ya chai katika shamba la chai la Uda Haupe mjini Kahawatte, Sri Lanka. Leelavathi ni mmoja wa mamia ya wakulima ambao wanatupilia mbali matumizi ya dawa za kuua magugu na kemikali zingine. Picha ni kwa hisani ya: Stella Paul/IPS

RATNAPURA, Sri Lanka, Machi 28, 2017 (IPS) - Siku inavyoendelea, Kamakandalagi Leelavathi anazama zaidi katika mistari inayovutia ya rangi ya kijani ya miti ya chai. Katika siku chache zilizopita, kumekuwa na radi kubwa. Mchunaji huyu wa majani chai mwenye umri wa miaka 55 amekuwa akivuna chai katika shamba la chai la Uda Houpe lililoko eneo la Hatton Sri Lanka. Mchunaji huyu anaharakisha kukamilisha kazi yake ya siku kabla ya kuanza kunyesha, siku hii anachuna kilogramu 22 ya majani chai.

“Ni vigumu kutabiri mvua siku hizi. Kwa sasa kuna mvua, lakini katika miezi michache iliyopita hakujakuwa na mvua, kulikuwa kumekauka sana,” Leelavathi ambaye ni mkulima anayemiliki shamba la ekari moja ambalo anategemea kupata riziki ya kila siku anaeleza.

Hata hivyo, katika shamba la chai ya Uda Houpe, hali ni bora zaidi, mwanaye Leelavathi, Daurkarlagi Taranga, na mkulima mwenzake wa chai anasema. "Hatujaathirika sana kama wengine. Hapa, miti ya chai bado ingali imejaa (majani ya chai) na ardhi bado ina unyevunyevu. Hali inayotokana na teknolojia tunayotumia," Taranga anaendelea kueleza.

Mbinu hizi ni mbinu zinazohifadhi ardhi ambazo wakulima wadogo wa chai wanaendeleza ili kutumia mashamba yao kwa njia ya kudumisha uchumi, Alluth Wattage Saman anaeleza. Saman ni meneja wa shamba la Uda Houpe. Mojawapo ya hatua muhimu miongoni mwa hatua zinazochukuliwa ni hatua ya kupunguza athari zinazoletwa na dawa za kuua magugu ambazo zinazingatiwa kama sababu kuu ya kuzorota kwa afya ya ardhi na miti ya chai katika eneo hilo.

Mchunaji chai katika shamba la chai la Bearwell nchini Sri Lanka ambalo linazingatia mbinu endelevu katika matumizi na usimamizi wa mfumo wake wa biashara. Picha ni kwa hisani ya: Stella Paul/IPS

Tishio la Mabadiliko ya Hali ya Hewa kwa Sekta hii yenye Faida kwa Wanasrilanka

Sekta ya chai nchini Sri Lanka imekuwepo kwa zaidi ya miaka 153 na bado ni sekta kubwa zaidi hivi leo. Sekta hii inawaajiri watu milioni 2.5. Kwa mujibu wa Bodi ya Maendeleo ya Sri Lanka, mazao ya sekta ya chai yanajumuisha asilimia 62 ya mauzo ya nje ya kilimo na huletea nchi dola bilioni 1.6 katika fedha za kigeni kila mwaka kama. Jamii ya wakulima wa chai 400, 000 wadogo wadogo inachangia katika biashara hii kubwa.

Hata hivyo, uchumi wa sekta ya ukuzaji wa chai unaoleta faida kwa nchi hii ya kisiwa umekumbwa na changamoto zinazokua za kimazingira- changamoto kubwa zaidi ikiwa ni kupunguka kwa ubora wa ardhi ya wakulima.

Kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Hali ya Jangwa Ulimwenguni (UNCCD), kuna kiwango cha juu cha uharibifu wa ardhi katika eneo la kukuza chai nchini Sri Lanka. Sababu kubwa ikiwa kwamba wakulima hapa wametumia dawa zilizotengezwa viwandani za kuua magugu katika mashamba yao kwa miongo kadhaa.

Wakulima hawa pia wameshughulikia kwa kiwango kidogo mno ulinzi wa vyanzo vya maji na viumbe hai karibu na mashamba. Hatua hii imeathiri kwa kiwango kikubwa afya ya udongo huku ikipunguza kiwango cha uwezo wa udongo kutoa mazao, hali inayofanya ardhi kuwa yenye asidi zaidi na kusababisha mmomonyoko wa udongo.

Huku uharibifu huu ukiathiri sekta nzima, maisha na usalama wa chakula wa wakulima wadogo wanaokuza chai yanaathirika zaidi, anasema Lalith Kumar ambaye ni meneja wa miradi katika Mamlaka ya Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai (Tea Small Holding Development Authority (TSHDA) huko Ratnapura. Eneo hili huzalisha zaidi ya asilimia 70 ya Chai nchini Sri Lanka.

Wachunaji chai katika shamba la chai la Bearwell nchini Sri Lanka ambalo linazingatia mbinu endelevu katika matumizi na usimamizi wa mfumo wake wa biashara. Picha ni kwa hisani ya: Stella Paul/IPS

Kunawirisha Mashamba wa Wakulima Wadogo Wadogo wa Chai

TSHDA ni shirika la serikali linalofanya kazi na wakulima wadogo wadogo wa chai nchini Sri Lanka. Kulingana na Kumar, kuna mashamba madogo 150 ya chai (chini ya ekari 10 za ardhi) katika eneo la Ratnapura pekee ambayo huwapa wakulima karibu rupee 100,000. Mabadiliko ya hali ya hewa yamefanya hali kuwa mbaya zaidi kwa kusababisha hali ya ukame mara kwa mara, mvua isiyo ya kawaida, na kuongeza kwa mmomonyoko wa udongo na ongezeko la kiwango cha asidi udongoni.

Matokeo yake ni miti ya chai kukauka na unyevunyevu kutoka sehemu ya juu ya ardhi, hali inayowacha udongo ukiwa umekauka na mizizi ya mimea kuwa dhaifu na kuharibiwa.

Ili kusaidia wakulima wa chai kukumbana na hali hii, TSHDA kwa sasa inafanya kazi na Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP) katika mradi wa kupunguza matumizi ya dawa za kuua magugu katika mashamba madogo na kubadilisha michakato ya uharibifu wa udongo kwa kuwaeleza wakulima kutumia mashamba yao kwa njia endelevu.

Lengo la mradi ni, "kuboresha mbinu za kutumia shamba ili ardhi iliyopo ya uzalishaji inakuwa na uwezo wa kuzalisha mazao zaidi na misitu, mito na sehemu zingine za ardhi zenye umuhimu wa kibaiolojia zilizo kwenye au karibu na maeneo yanayokuza chai zinalindwa dhidi ya athari mbaya.” Maelezo haya ni kwa mujibu wa maelezo ya Global

Environment Facility (GEF), ambaye ni mfadhili wa mradi huo unaogharimu rupee milioni 2.9. Hatua kuu inayochukuliwa na TSHDA ni kufundisha wakulima kutumia ardhi yao kwa njia endelevu yenye matumizi madogo au isiyotumia dawa za kuua magugu.

"Tumeanza kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa mashamba madogo madogo kuhusu mbinu endelevu za usimamizi wa ardhi ambazo ni rahisi lakini zina manufaa," Kumar alisema. Magugu mengi hukua na kuzingira miti ya chai, lakini baadhi ya magugu haya huwa hayana madhara.

"Tunawafundisha jinsi ya kutambua magugu na kuyaondoa magugu yenye madhara aidha kwa kuyang'oa ardhini au kuyakata kwenye mizizi. Magugu yanayoondolewa hutumiwa kwa kukusanywa pamoja na kuwekwa ili kuleta unyevunyevu. Magugu yaliyokusanywa huwekwa kati ya safu mbili za miti ya chai. Hii husaidia kurejesha unyevunyevu udongoni," Kamar alieleza.

Kutoa Mafunzo kwa Jamii

Saman, meneja wa Uda Haupe, ni mmoja wa wakulima wadogo 300 wa chai ambao wamefundishwa na TSHDA kufikia sasa. Saman anaeleza kwamba mafunzo yalikuwa mafunzo yasiyo rasmi, yaliyowaonyesha wakulima hatua za kufanya na mafunzo ambayo yalijumuisha ziara ya siku moja katika shamba linalosimamiwa kwa njia endelevu inayoleta manufaa - shamba hili lilikuwa shamba la chai la Hapugastenne.

Katika shamba hilo, Saman aliona wakulima wadogo kama yeye wakitumia mashamba yao bila dawa za kuua magugu na wadudu zinazotengenezwa viwandani. Pia alijifunza jinsi ya kutumia mbolea inayotokana na mabaki asilia wala si mbolea inayotengenezwa viwandani, kulinda vyanzo vya maji kama chemchemi asili za maji zilizo katika shamba hilo la chai pamoja na miti inayotoa kivuli ili ndege na wanyama wengine pia waweze kuishi. Hatimaye, alijifunza kuwa mazao ya shamba hili yalikuwa yameongezeka karibu asilimia 60 tangu walipoanza kutumia mbinu hizo.

Mkulima huyu anasema kuwa ziara hiyo ilinisaidia kutambua, "hatua ndogo zinazoweza kuleta mabadiliko makubwa katika shamba langu".

Matokeo yake yanatia moyo, "Hapo awali nilikuwa ninatumia rupee 35,000 kila mwaka kununua dawa za kuua magugu, kwa sasa ninaweka kiasi hicho cha pesa kama akiba. Faida yangu ya jumla imepanda kwa hadi rupee 75,000," anasema Saman, ambaye ameshiriki ujuzi wake mpya na wafanyakazi wake.

Baadhi ya Vikwazo ambavyo Havijashughulikiwa

Saman na wakulima wengine wadogo wa chai katika eneo la Ratnapura kama Leelavathi huuza mazao yao ya chai kwa Shamba la Kahawatte, shamba la chai linalomilikiwa na shirika la Dilmah. Mapema mwezi huu, shamba hilo lilipokea Cheti cha Rainforest Alliance ambacho hutambua shamba linalodumisha viwango endelevu katika mfumo wake wa biashara ikiwemo mashamba ambayo Dilmah hununua majani yake ya chai. Hatua hii tayari imeongeza bei ya mazao ya chai ya shamba hilo lakini wauzaji kama Saman hawafahamu umuhimu wa cheti hicho au manufaa yake ya kiuchumi kama vile thamani kubwa ya chai la shamba hilo sokoni.

"Hakuna mtu ambaye ametueleza kuhusu hili," Saman anasema.

Wakulima Wengine wanataka serikali kuwasaidia kwa kuwapa fedha ili wakabiliane vyema zaidi na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa.

Kwa sasa, TSHDA inatoa asilimia 50 ya punguzo kwa wakulima ambao wangependa miti yao ya chai kupandwa upya kwenye mashamba yao - hatua ambayo huwa ngumu inayogharimu gharama ya juu, hatua hii hujumuisha kungo'a miti yote ya chai, kuandaa mchanga upya na kupanda miti mingine midogo ya chai.

Hii inafanywa wakati mavuno katika shamba yanapungua kwa kiwango kikubwa aidha kutokana na miti kuzeeka (kwa kawaida miti ya chai huwa ni miaka 30 au zaidi) au uharibifu mkali wa ardhi ambao unazuia uwezo wa ardhi kutoa mavuno. Hata hivyo, hakuna ruzuku nyingine au motisha inayotolewa kwa wakulima kwa sasa kwa wao kuchukua hatua za kudumisha matumizi endelevu na usimamizi endelevu wa ardhi kwenye mashamba yao - sera ambayo wakulima wadogo wa chai kama vile Leelavathi wangependa kuona ikibadilishwa.

"Kutokana na matumizi ya magugu kudumisha unyevunyevu ardhi, nilianza kuokoa rupee 700 kila mwezi kwa sababu sikununua dawa za kuua magugu na mapato yangu yote yaliongezeka hadi rupee 15,000. Lakini kwa sababu ya ukame unaoongezeka, ninahitaji kutumia kiasi kikubwa cha pesa hizo kununua mbolea nyingi. Ikiwa serikali itatoa ruzuku, itasaidia sana. Au labda itanibidi nihamie kwenye shamba lingine kubwa la chai ili niweze kupata mapato zaidi," Leelavathi anasema.